

Taarifa ya Malengo: Tunaitumikia jumuia na kuifanyia mipango wakati wa kuchanganua na kufaana na mahitaji ya siku za mbele.

Maadili ya FM

Heshima

Tunawathamini washiriki wote wa jumuia yetu kwa kutambua na kuheshimu jinsi tunavyofanana na jinsi tunavyotofautiana.

- Ninatambua adhamu ya kibinadamu ya kila mtu na hujaribu kuwatendea wote kwa fadhili, huruma na rehema.
- Ninajitahidi kupitia mizozo kwa njia ya kujenga mapatano.
- Mimi hushirikiana na wengine kwa weledi, na huwa ni mwenye ufikirio kwa maneno na matendo yangu.

Utimilifu

Sisi hufuatia haki, husema mambo wazi, na kutenda kwa haki katika wasiliano na wengine.

- Mimi hujaribu kufuatia malengo na maadili ya Chuo Kikuu katika kazi yangu.
- Mimi ni mwaminifu kwa maneno na matendo yangu.
- Natamani kufanya jambo lililo sawa hata kama si rahisi kufanya hivyo.
- Nakubali matokeo ya matendo yangu.

Usimamizi

Sisi husimamia mipango ya rasilimali zilizotukabidhi kwa uangalifu na busara.

- Mimi hujaribu kutafuta njia za kupunguza matokeo mabaya ya kimazingira yaliyoletwa na Chuo Kikuu cha Virginia.
- Mimi hujaribu kuyaacha majengo na eneo la Chuo Kikuu katika hali bora kuliko yaliyokuwa kwanza.
- Mimi huchagua nyenzo zinazofaa na taratibu bora ili kufanya kazi yangu.
- Nachukua madaraka ya kufanya kazi kwa usalama.

Ushirikiano

Sisi hupata nguvu zaidi tukifanya kazi kwa kushirikiana ili kuunga mkono malengo ya Chuo Kikuu.

- Mimi huzungumza kwa njia inayolewaka nikishirika habari na wenzangu.
- Niko tayari kupokea mawazo na taratibu za wengine.
- Mimi hushauriana na wengine ili kutafuta masuluhisho ya matatizo.
- Mimi huthamini kazi njema bila kujali ni nani aliyeifanya.